## FUNZO LA 9

1. Je, Mungu alimaliza kuumba mbingu na nchi?
-Ndiyo.

2. Kwa nini Mungu humalizia kazi ambayo ameanzisha?
-Kwa sababu Mungu habadiliki.
-Kwa sababu hakuna chochote kinachoweza kumzuia Mungu kumaliza kazi yake.

3. Wakati Mungu anapoanza kazi yake, je Shetani na mapepo wanaweza kuisimamisha?
-La.

4. Kwa nini Mungu alipumzika siku ya saba?
-Kwa sababu Mungu alikuwa amemaliza kuumba kila kitu alichokuwa amekipanga kuumba.

5. Mungu aliumba vitu vyote kwa siku ngapi?
-Siku sita pekee.

6. Kama hatukuwa na mvua hapo mwanzo, je Mungu aliinyunyizia aje nchi maji?
-Mungu alinyunyizia nchi maji kutokana na ukungu uliotoka ardhini.

7. Jina ya bustani iliyopandwa na Mungu ni?
-Bustani ya Edeni.

8, Mungu alimpandia nani bustani ya Edeni?



-Adamu.

9. Kwa nini Mungu alimpandia Adamu bustani ya Edeni?
-Kwa sababu Mungu alimpenda Adamu sana.

10. Kwa nini Mungu hakumwuliza Adamu kama angemweka kwenye bustani ya Edeni?
-Kwa sababu Mungu alimuumba Adamu, Adamu alikuwa wa Mungu.

11. Kwa sababu Mungu aliwaumba wanadamu wote, wanadamu wote ni wa nani?
-Wanadamu wote ni wa Mungu.

12. Jina la mti wa kwanza ambao Mungu alipanda katikati ya bustani ya Edeni ni lipi?
-Mti wa Uzima.

13. Kwa nini Mungu aliupanda mti wa uzima katikati ya bustani ya Edeni?
-Mungu alimtaka Adamu ale matunda ya mti huo ili aishi milele.

14. Jina la mti wa pili ambao Mungu aliupanda katikati ya bustani ya Edeni ni lipi?
-Mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

15. Kuhusu mti wa ujuzi wa mema na mabaya, ni amri ipi Mungu alimpa Adamu?
-Mungu alimwamuru Adamu asile matunda ya mti huo.

16. Kama Adamu angekula tunda la mti wa ujuzi wa wema na mabaya, nini kingemfanyikia?
-Adamu angekufa.

17. Kifo ni nini?
-Kutenganishwa na Mungu ambaye anapeana uhai.
-Kutenganishwa kwa nafsi na mwili.
-kutenganishwa milele kwenye ziwa la moto wa milele.

-Tusome kile Mungu alisema baada ya kumuumba Adamu:

Tusome Mwanzo 2:18

18-Kisha BWANA Mungu akasema, "Si vizuri huyu mwanamume kuwa peke yake. Nitamfanyia msaidizi wa kumfaa."

-Mungu aliamua kuwa Adamu hangeishi peke yake.
-Mungu aliamua kumuumbia Adamu mke.

-Mungu hakumuuliza Adamu kile alichokitaka.
-Mungu ndiye aliyeamua kumuumbia Adamu mke.

-Kwa nini Mungu akaamua kumuumbia Adamu mke?

-Kwa sababu Mungu alimpenda sana Adamu.
-Kwa sababu Mungu hakutaka Adamu awe peke yake.

Tusome Mwanzo 2:19-20a



19-BWANA Mungu akaumba kila mnyama wa porini na kila ndege wa angani, halafu akamletea huyo mwanamume aone atawapa majina gani; na majina aliyowapa viumbe hao, yakawa ndiyo majina yao.
20-Basi, huyo mwanamume akawapa majina wanyama wote wa kufugwa, wanyama wa porini na ndege wote wa angani.

-Hapo mwanzo Mungu alimpa Adamu mamlaka juu ya nchi.
-Hapo mwanzo Mungu alimpa pia Adamu mamlaka juu wanyama wote.

-Mungu alimwambia Adamu kuwapa majina wanyama wote.

-Kwa hivyo Adamu aliwapa wanyama wote majina.

-Lakini Adamu alikuwa mwanadamu pekee nchini.

Tusome Mwanzo 2:20b

20-Lakini hakupatikana msaidizi yeyote wa kumfaa.

-Je, Mungu aliwaumba wanadamu na wanyama sawa?
-La.

-Je, Mungu aliumbaje wanadamu na wanyama tofauti?

-Mungu hakuumba wanyama kwa mfano wake.

-Mungu aliwaumba wanadamu pekee kwa mfano wake.

-Wanadamu waweza wakamjua Mungu lakini wanyama hawawezi.
-Wanadamu waweza wakampenda Mungu lakini wanyama hawawezi.
-Wanadamu waweza wakamchagua Mungu lakini wanyama hawawezi.

-Ikiwa Adamu angefikiria jambo fulani, je angeweza kuwauliza wanyama wafikirie naye?
-La.

-Ikiwa Adamu angekuwa na furaha au huzuni, je angeweza kuwauliza wanyama wawe na furaha au huzuni pia?
-La.

-Ikiwa Adamu angetaka kuchagua kitu cha kufanya, je angeweza kuwauliza wanyama ikiwa wangechagua kufanya naye kitu hicho?
-La.

-Je, wanyama walikuwa wasaidizi wazuri kwa Adamu?
-La.

-Adamu alihitaji msaidizi mzuri ambaye angeongea naye.

-Kwa sababu Mungu alimpenda Adamu, aliamua kumuumbia Adamu mke.

-Je, Adamu angeweza kujiumbia mke?
-La.



-Je, Shetani na mapepo wake walikuwa na uwezo wa kumuumbia Adamu mke?
-La.

-Nani pekee aliweza kumuumbia Adamu mke?
-Mungu.

-Siku moja, Mungu alimuumbia Adamu mke.

Tusome Mwanzo 2:21-22

21-Basi, BWANA Mungu akamletea huyo mwanamume usingizi mzito, na alipokuwa usingizini, akatwaa ubavu wake mmoja na kupafunika mahali pale kwa nyama.
22-Na huo ubavu BWANA Mungu alioutoa kwa yule mwanamume akaufanya kuwa mwanamke, akamleta kwa huyo mwanamume.

-Mungu pekee ndiye aliyekuwa na uwezo wa kumwumbia Adamu mke.

-Nguvu za Mungu haziishi.
-Hakuna chochote kinachomshinda Mungu.

-Mungu alimuumba mwanamke wa kwanza na akampa kama zawadi kwa Adamu.

-Ukipewa zawadi nzuri na mtu fulani, je utaitunza vyema?
-Ndiyo.

-Ukipewa ng'ombe na mtu, utamlinda vyema?
-Ndiyo.

-Ukipewa gari na mtu, utailinda vyema?
-Ndiyo.

-Mungu alimuumba mwanamke wa kwanza na kumpa kama zawadi nzuri kwa Adamu.

-Mungu alimtaka Adamu amtunze vyema mke wake.
-Mungu alimtaka Adamu ampende zaidi mke wake.

-Tusome kilichosemwa na Adamu wakati Mungu alimpa mke:

Tusome Mwanzo 2:23-24

23-Ndipo huyo mwanamume akasema, "Naam! Huyu ni mfupa kutoka mifupa yangu, na nyama kutoka nyama yangu. Huyu ataitwa 'Mwanamke,' kwa sababu ametolewa katika mwanamume."
24-Ndiyo maana mwanamume humwacha baba yake na mama yake, akaambatana na mkewe, nao wawili huwa mwili mmoja.

-Mungu alimuumbia mwanamume mwanamke ili wakaoane.
-Mungu alimuumbia mwanaume mwanamke ili waishi pamoja.
-Mungu alimuumbia mwanamume mwanamke ili wazae watoto.

-Chochote anachofanya Mungu ni kizuri.



-Chochote anachofanya Mungu ni kikamilifu.
-Hii ni kwa sababu Mungu ni mwema na mkamilifu.

-Mungu hawezi kufikirii maovu yoyote.
-Mungu hawezi kunena maovu yoyote.
-Mungu hawezi kufanya maovu yoyote.

-Je, unafikiri Adamu alikuwa na furaha kwa kupokea zawadi kuu ya mke?
-Ndiyo.

-Adamu alikuwa na furaha sana.

-Jina la mkewe Adamu ni lipi?
-Jina la mkewe Adamu ni Hawa.

Tusome Mwanzo 2:25

25-Huyo mwanamume na mkewe wote walikuwa uchi, lakini hawakuona haya.

-Hapo mwanzo, Adamu hakuona haya.
-Hapo mwanzo, Hawa pia hakuona haya.

-Hapo mwanzo, Mungu aliwaumba Adamu na Hawa wakamilifu.
-Hapo mwanzo, Adamu na Hawa hawakujua maovu.

-Hapo mwanzo, Adamu na Hawa walitembea na Mungu na walikuwa na furaha sana.